# BUNGE LA TANZANIA

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 10 Aprili, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili katika Mkutano wake wa Sita, pamoja na shughuli nyingine, lilipitisha Miswada mitano ya Sheria ya Serikali. Miswada hiyo, baada ya kukamilika katika hatua zake zote za uchapishwaji, ilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kupata Kibali chake. Ninafurahi kulifahamisha Bunge letu Tukufu kwamba, Mheshimiwa Rais, ametoa kibali hicho na Miswada hiyo sasa ni Sheria za nchi kama ifuatavyo: *The Business Activities Registration Act*, 2007 Namba 14; *The Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act*, 2007, ambao unakuwa Namba 15; *The Judges Remuneration and Terminal Benefits Act*, 2007 Namba 16; *The Deep Sea Fishing Authority (Amendment) Act*, 2007 Namba 17; na *The Law School of Tanzania Act*, 2007 Namba 18 wa 2007. *(Makofi)*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Mjumbe afuataye aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, nina hakika, mtapenda nimpongeze Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge mpya wa Jimbo la Tunduru. Nadhani kazi ilikuwa kubwa, lakini faraja ni kwamba, sasa amefikia hali ya Ubunge, kihalali kabisa. Anayo idhini ya Spika, hata leo hii anaweza kuuliza swali la nyongeza. Bahati iliyoje, kwa taarifa yake tu, kiti alichokwenda kukalia ni kile alichokuwa akikaa Mheshimiwa William M. Ngeleja, kwa hiyo, inaashiria mambo mema. *(Makofi/Kicheko)*

## HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali, pamoja na nyongeza zake, zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

**Wito wa Viongozi wa Mikoa Kumi – Dar es Salaam**

**MHE. KABWE Z. ZITTO (k.n.y. MHE. MHONGA S. RUHWANYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 9 hadi 20 Januari, 2007, uliitishwa Mkutano wa Viongozi/Watendaji wa Mikoa kumi ya Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Mtwara, Tabora, Dodoma, Kagera, Kilimanjaro na Pwani, iliyoshindwa kupeleka Sekondari zaidi ya asilimia 50 ya wanafunzi waliofaulu Mtihani wa Darasa la Saba mwaka 2006 ili kupanga mikakati ya kupeleka wanafunzi wengi sekondari kwa zaidi ya asilimia 75 ya wanafunzi waliofaulu mwaka 2006:-

(a) Kwa kuwa jambo hilo, lilikuwa la dharura, je, kwa nini viongozi hao wasingepewa maagizo hayo kwa njia ya vyombo vya habari kama redio na televisheni ili waweze kutekeleza jambo hilo mara moja, badala ya kusafiri nje ya vituo vyao vya kazi kwa karibu majuma mawili na baadaye wapewe maandishi kama mwongozo katika utekelezaji agizo hilo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitumika kama nauli, posho ya malazi na chakula, kwa muda wote viongozi hao walipokuwa nje ya vituo vyao vya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi:-

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa hotuba yake ya kuuaga mwaka 2006 na kuukaribisha mwaka 2007, mnamo tarehe 31 Desemba, 2006. Katika hotuba yake, aliagiza mambo yafuatayo, ninanukuu:-

“Mwaka huu wa 2006 wamefaulu wanafunzi 468,181. Kama nafasi za sekondari zitabaki idadi hii hii kwa mwaka ujao wa 2007, vijana 224,828 watakosa nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari. Idadi hii itateremsha kiwango chetu cha mafanikio kutoka asilimia 79.8 ya mwaka jana hadi asilimia 52. Nataka kuongeza sauti yangu kwa

Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Viongozi wa Halmashauri za Wilaya na Miji, pamoja na Viongozi wa Tarafa, Kata na Vijiji, tujitahidi kufanya kila tuwezalo kuhakikisha kuwa, hatushuki kuliko pale tulipofikia mwaka huu wa 2006." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshemiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliona ni busara kukutana na Mikoa, ambayo ilikuwa inapeleka wanafunzi chini ya asilimia 50. Hivyo, mnamo Januari, 2007, Serikali iliitisha kikao cha Viongozi na Watendaji wa Mikoa kumi na moja na siyo kumi kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge, ili kuweka mikakati ya kufikisha asilimia zaidi ya 75 ya wanafunzi waliofaulu kuingia Kidato cha Kwanza.

Mheshimiwa Spika, kila Mkoa ulipangiwa siku na saa ya kukutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuelezea mikakati yake na walipomaliza walirejea katika vituo vyao vya kazi, kuendelea na majukumu yao na hawakukaa Dar es Salaam kwa muda wa wiki mbili, kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza. Aidha, ziko njia mbalimbali za kupeana taarifa na maelekezo, kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge. Kwa hili, kulikuwa na ulazima wa mazungumzo ya ana kwa ana, kati ya Viongozi na Watendaji wa Mikoa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri walioshiriki katika kikao hicho, kwa kufafanua sera, miongozo na kuweka mikakati ya upatikanaji wa fedha zinazohusiana na suala zima la elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Mikoa, walikuja na mapendekezo ambayo kwa njia nyingine, yasingeweza kufahamika kwa urahisi na hatimaye kufikia muafaka kwa njia za redio au televisheni zingetumika. Kwa mfano, baadhi ya Halmashauri, zilikuwa na matatizo ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi au kuwe na madarasa ambayo yalijengwa katika shule ambazo tayari zilikuwa na mikondo minne kulingana na ukubwa wa shule. Hivyo, ufafanuzi wa sera na miongozo, uliotolewa katika vikao hivyo kwa viongozi hao. Hii iliwapa nguvu mpya ya kwenda kuboresha mikakati yao na wote walifanikisha. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, viongozi hao wa ngazi ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri, walijigharamia kutokana na mafungu ya Mikoa na Halmashauri, nauli na posho ya kujikimu, ambayo inajumuisha chakula kwa siku walizokaa Dar es Salaam, kuhudhuria kikao hicho kwa siku walizopangiwa. Jumla ya gharama hizo kwa mikoa yote kumi na moja ni kama ifuatavyo:-

Posho ya kujikimu kwa jumla ya mikoa yote 11 ni shilingi milioni 91.0, nauli na mafuta shilingi milioni 63, vifaa mbalimbali *(stationeries)* na kadhalika shilingi 5,000,000; jumla kuu shilingi milioni 160.1 zilitumika.

Mheshimiwa Spika, matunda yaliyotokana na kikao hicho ni makubwa, ikilinganishwa na gharama zilizotajwa hapo juu, kwani kabla ya vikao hivyo ni

wanafunzi 116,680 waliokuwa wamepata nafasi ya kujiunga na masomo ya sekondari katika mikoa hiyo kati ya wanafunzi 268,702 waliokuwa wamefaulu.

Baada ya majadiliano na msukumo uliowekwa na Viongozi wa Kitaifa, Mikoa, Wilaya na Halmashauri husika, wanafunzi 123,279 walipatiwa nafasi ya kujiunga na masomo katika sekondari zilizojengwa na wananchi katika Mikoa hiyo kumi na moja. Idadi hii ikijumlishwa na ile idadi ya mwanzo, jumla ya wanafunzi 239,959 walijiunga na masomo ya sekondari hadi sasa kwa Mikoa hiyo 11. Kitaifa tumepanda kutoka asilimia 52 hadi kufikia asilimia 89. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, napenda kuwapongeza viongozi katika ngazi mbalimbali na wananchi, kwa juhudi kubwa zilizooneshwa katika suala zima la kuwapatia watoto wetu nafasi ya masomo katika shule zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, pamoja na Serikali. Pongezi za pekee, ziende kwa Mikoa ile mitano, ambayo imepeleka wanafunzi kwa asilimia 100. Mikoa hiyo ni pamoja na Tabora, Shinyanga, Dodoma, Singida na Arusha. Pia nazipongeza zile Wilaya zote, ambazo zimepeleka wanafunzi kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake marefu sana.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ya Awamu ya Nne, inaanza kazi yake, iliwachukua Wakuu wa Mikoa wote na Wakuu wa Wilaya wote na kuwapa semina elekezi, ambazo naamini kabisa, ndio zilizoweza kuwapa maelekezo ya sera na mipango mbalimbali ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Je, kulikuwa kuna haja gani kwa Serikali kutumia shilingi milioni 160 kwa ajili ya kutoa maelekezo mapya kwa Wakuu wa Mikoa, kuhusiana na shule za sekondari; wakati hizo shilingi milioni 160 zingeweza kutengeneza jumla ya madarasa 20; sasa huoni kwamba, haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali, ambazo zimepangwa katika mafungu ya Mikoa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu kwa kweli Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na wengine wanaofikiria hivyo, kwanza, kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ambayo imefanyika. Lakini hata hivyo, naomba niseme tu kwa upande mwingine, Waziri Mkuu, ndiye Kiongozi wa shule zote za Serikali. Mimi sidhani kama itakuwa ni sahihi, kumwelekeza ni namna gani, aongoze Serikali yake wakati wa kutekeleza majukumu yake. Kazi iliyofanyika na mimi nashangaa kwamba, mnaulizia suala hili kwa maana hii tu, lakini Naibu Mawaziri, tumewapeleka nao kwenda kuangalia na kusukuma jambo hili kwa nguvu sana. Mimi na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tulikwenda vilevile katika kujaribu kujiridhisha na shughuli inavyokwenda. Kwa kifupi tunasema, gharama zilizotumika ukilinganisha na kazi kubwa iliyofanyika ya kujenga shule zaidi 640, ndani

ya kipindi hiki kifupi, huwezi ukalinganisha hata kidogo na gharama ya shilingi milioni 160. Kwa hiyo, nataka kwa kweli nitumie nafasi hii, kurudia kuzipongeza sana Halmashauri zote na Viongozi wote wa Mikoa, kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. *(Makofi)*

Na. 2

**Sheria Namba 7 na 8 ya Mwaka 1982**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria Namba 7 na 8 ya mwaka 1982, inayohusu Uchaguzi wa Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Meya kwenye Manispaa, imepitwa na wakati hasa katika kipengele kinachohusu Mwenyekiti/Meya wa Manispaa kukaa madarakani kwa muda wa miaka mitano; na kwa kuwa sheria hiyo ilitungwa wakati wa mfumo wa Chama kimoja cha siasa na sasa tuko katika mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa;

Je, inapotokea kuwa baadhi ya Madiwani kwenye Halmashauri/Manispaa wamejiuzulu na kusababisha Uchaguzi Mdogo kufanyika, hakuna uwezekano mkubwa kwa Madiwani watakaochaguliwa tena, wakawa si wale waliomchagua Mwenyekiti au Meya na hivyo kusababisha malumbano ya maamuzi katika vikao vyao na hivyo kukosekana kwa *majority support* kwenye Baraza la Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mbunge wa Chalinze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria Namba 7 na 8 za mwaka 1982, zimekuwa zinafanyiwa marekebisho mbalimbali, ili kukidhi mahitaji na kuzingatia mabadaliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, yanayotokea. Aidha, Sheria hizo zimefanyiwa marekebisho makubwa mwaka 1999 na marekebisho ya pili yamefanywa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Serikali za Mitaa Namba 13 ya mwaka 2006. Marekebisho haya, yamezingatia mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa na mabadiliko ya sera za kiuchumi na kijamii. Hivyo, naomba nisikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Sheria hizo zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mdogo wa Diwani, unafanyika baada ya nafasi ya Udiwani kuwa wazi, kutokana na Diwani kujiuzulu, kufa, kufukuzwa uanachama kutoka chama chake cha siasa na kukosa kuhudhuria vikao au kuwa na kosa la jinai.

Mheshimiwa Spika, ingawa Meya na Mwenyekiti wa Halmashauri, huchaguliwa kupitia vyama vyao vya siasa, Mwenyekiti au Meya, akishachaguliwa anakuwa Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri nzima hivyo, Madiwani watakaochaguliwa baadaye katika

Uchaguzi Mdogo, wanatakiwa kuheshimu uamuzi wa Madiwani wenzao, waliomchagua Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spia, suala la Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri kukosa *majority support*, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uamuzi unaotokana na vikao katika Halmashauri, kuzingatia Sera za Kitaifa, Sheria na manufaa ya maamuzi hayo, kwa wananchi wa Halmashauri na Taifa kwa ujumla na siyo *majority support* ya Mwenyekiti au Meya.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa suala hili hutokana na hali inayojitokeza kila siku, Diwani anakufa yuko katika nafasi ya Udiwani, Mbunge anakufa yuko katika nafasi ya Ubunge, lakini Mbunge au Diwani yule ni Chama cha Mapinduzi, tumetoka jasho kumpata; sasa akifa atoke tena Diwani mwingine kutoka chama kile bila ya kuwa na uchaguzi mwingine; je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba, tangu sasa Diwani wa chama chochote akifa, basi hakutakuwa na uchaguzi, ila chama kile kitatoa Diwani badala ya yule aliyefariki? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la ndugu yangu, Mheshimiwa Profesa Idris A. Mtulia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masuala haya ya demokrasia ni vizuri yakazingatia misingi ambayo ni muhimu sana. Moja ya jambo ambalo muda wote tutaendelea kulihimiza ni upatikanaji wa viongozi, kwa utaratibu wa kuchaguliwa. Kama Diwani wa kwanza aliingia madarakani kwa kuchaguliwa kisheria na kwa kweli hata misingi ya demokrasia ndivyo inavyotaka. Atakayekuwa anakuja kuchukua nafasi ya huyo ambaye sasa hayupo, ni vizuri vile vile akatumia utaratibu huo huo ili kukidhi matakwa ya wapiga kura. Vinginevyo tutakuwa tunaamini juu juu tu kwamba, bila shaka huyu ndiye anayekubaliwa. Imetokea mara nyingi tu kwamba, aliyekuwa pengine amefuatia, siyo lazima akawa ndiyo mshindi. Kwa hiyo, ni vizuri tukaendeleza jambo hili kwa nia nzuri tu. *(Makofi)*

Na. 3

**Ubovu wa Barabara Muhimu – Serengeti**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara muhimu za Wilaya ya Serengeti mfano barabara za kutoka Sirori, Simba hadi Rung'abure, Mto Mara hadi Magumu, Mto Mara hadi Iramba, Mugumu hadi *Fort Ikoma* ni za udongo na huharibiwa na mvua wakati wa masika, hali iliyosababisha kero kubwa sana ya usafiri kwa wananchi wa Wilaya ya Serengeti:-

(a) Je, ni lini Serikali itazitengeneza barabara hizo kwa kiwango cha changarawe au lami?

(b) Je, kazi hiyo itagharimu kiasi gani cha fedha na itaanza lini?

(c) Je, kazi ya kutengeneza barabara ya kutoka Musoma kupitia Natta, Mugumu hadi Arusha, kwa kiwango cha lami itaanza lini na itagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sirori – Simba – Rung'abure, yenye urefu wa kilomita 50 ni sehemu ya barabara ya Mkoa inayojulikana *R185.* Nyankanga – Sirori Simba – Rung'abure yenye urefu wa kilomita 91 na sehemu ya Mto Mara hadi Mugumu yenye urefu wa kilomita 29 ni sehemu ya barabara ya Mkoa *R183* ya Tarime – Natta yenye urefu wa kilomita 123. Aidha, barabara ya Mugumu hadi *Fort Ikoma* (Kilomita 31) na sehemu ya barabara toka Mto Mara hadi Majimoto, kwa sasa ni barabara za Wilaya. Sehemu ya Iramba hadi Majimoto (Kilomita 13) katika barabara ya Mto Mara – Iramba inahudumiwa na Wizara yangu, kupitia Wakala wa Barabara *(TANROAD)* na sehemu iliyobaki iko chini ya uangalizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, uwezo wa Serikali kibajeti ni mdogo. Hivyo, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuzitengeneza barabara hizo, ikiwa ni pamoja na zile zinazohudumiwa na Wizara yangu, nilizozitaja kwa kiwango cha lami au changarawe. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuzihudumia barabara hizo ili zipitike bila matatizo makubwa.

(b) Hatuwezi kujua kiasi cha fedha kinachotakiwa hadi upembuzi yakinifu na usanifu viwe vimefanyika. Aidha, muda wa kukamilika, utategemea pia upatikanaji wa fedha.

(c) Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kutaka kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kutoka Musoma – Natta – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu. Hadi sasa Serikali imechukua hatua zifuatazo: Usanifu wa kina wa sehemu ya barabara ya Musoma hadi *Fort Ikoma* umekamilika; Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kati ya Mugumu – Loliondo hadi Mto wa Mbu, unaendelea. Mhandisi Mshauri, anategemea

kukamilisha kazi hiyo mwishoni mwa mwezi wa Mei, 2007. Gharama ya mradi mzima itajulikana baada ya kukamilisha kazi hizo. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu, lakini nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kipande cha barabara toka Mugumu hadi *Fort Ikoma* ni muhimu sana katika kuunganisha mkoa wetu na Arusha na vile vile kuunganisha Mkoa wetu na Kenya na kipande hiki kimekuwa kinaharibika, sasa inabidi magari yatoke Arusha - Natta, yapande kuja Mugumu, ambayo ni karibu km 80. Je, ni kwa nini kipande hiki kifupi, kisitengenezwa kiwekwe chini ya *TANROAD* ili kiwe kinapewa hela za kutosha na kuzuia watu kuzunguka Kenya wakati wa masika? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, barabara hiyo ya kutoka Mgumu hadi *Fort Ikoma* imeshaombewa hata na Mkoa ipandishwe hadhi, ishughulikiwe na *TANROAD,* kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha kwa kupitia Tarime, Serengeti hadi Arusha. Ombi hili linashughulikiwa, katika marekebisho ya barabara zetu, litazingatiwa suala hilo kwamba, kati ya Mgumu na *Fort Ikoma* (km 31), sasa iingie kwenye barabara ya Tarime - Mugumu - *Fort Ikoma* kuelekea Serengeti na ihudumiwe na *TANROAD.*

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, nakumbuka hiyo barabara ya Arusha - Musoma, imeharibika sasa imefungwa kwa muda usiopungua miezi sita na matokeo yake gharama za mizigo zimepanda zaidi ya mara mbili. Lakini kwa bahati nzuri, baada ya kuwa barabara imetengemaa, hadi sasa magari hayajaruhusiwa kupita katika barabara hiyo. Nataka kujua itachukua muda gani kuruhusu magari yapite ili ule unafuu waliokuwa wanaupata wananchi wa Musoma, waweze kuupata kuliko ambavyo sasa gharama zimepanda zaidi ya mara mbili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ukweli kazi ya Wizara yetu chini ya *TANROAD,* ilikuwa ni kurekebisha barabara hiyo iweze kupitika. Sasa suala kwamba, mabasi bado hayajaanza kupita, mimi siwezi kuwa na hakika, ni mamlaka gani imezuia, kama ni wenye mabasi wenyewe bado kuna kitu wanaogopa sijaelewa, labda tutafanya mawasiliano tujue ni nini. Kama tumesharekebisha barabara ni mategemeo yetu kwa kweli kwamba, mabasi sasa yaanza kufanya kazi. Labda tulifuatilie hilo mimi na yeye, katika ngazi ya Mkoa wa Mara, tuweze kujua kwa nini wenye mabasi hawajaanza kazi katika barabara hiyo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii, niweze kuuliza swali la nyongeza. Lakini kabla sijauliza swali, naomba nitumie nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kupata ushindi wa kishindo katika Jimbo la Tunduru. Napenda pia kuwapongeza na

kuwashukuru wananchi wote wa Wilaya ya Tunduru, kwa kutupatia CCM ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Kwa kuwa barabara za Wilaya ya Serengeti zinafanana na matatizo ya ubovu wa barabara za Mkoa wa Ruvuma, hasa katika barabara kuu itokayo Masasi - Tunduru - Namtumbo - Songea mpaka Mbinga;

Je, Serikali inaweza kuwaeleza nini wananchi wa Wilaya hasa za Tunduru na Namtumbo? Barabara hiyo, itaanza utekelezaji wake lini, tukitilia maanani kuwa iko katika mpango wa utekelezaji wa Serikali? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ni kama jipya, lakini nadhani kwa umuhimu na uzito wa barabara hii na uwezo mkubwa alionao Naibu Waziri kufahamu miundombinu ya nchi nzima, naliruhusu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, barabara hiyo imekuwa ni kero ya muda mrefu na ndiyo maana jitihada kubwa zimefanyika kuhakikisha kwamba barabara hiyo inaanza kujengwa.

Mheshimiwa Rais toka wakati wa kampeni mpaka hivi sasa, Mheshimiwa Mbunge, amekuwa akisisitiza na kuhangaika kusaidiana na Serikali, namna ya kujenga barabara hiyo kutoka Masasi - Tunduru kupitia Namtumbo - Songea - Mbinga mpaka *Mbamba Bay.*

Nataka kuwahakikishia wananchi wa Mikoa hiyo kwamba, Serikali ina nia thabiti na hivi karibuni tayari imeanza kutengezwa kwa vipande vipande, kwa sababu barabara ni ndefu na tumeshakubaliwa kupata fedha kwenye maeneo fulani, kuanzia Masasi kwenda hadi Mangaka na sasa hivi tunazungumza tuanzie pale tuendelee mpaka Tunduru na baadaye tufike Songea - Mbinga - *Mbamba Bay.* Tunawahakikishieni kwamba, barabara hiyo ni *priority* katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika ujenzi wa barabara nchini. *(Makofi)*

Na. 4

**Ujenzi wa Gati la Kyamkwikwi**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika bajeti za miaka 2004/2005 na 2005/2006 Serikali ilikubali kujenga Gati ya Kyamkwikwi katika Wilaya ya Muleba, ahadi iliyojenga matumaini ya kuboresha usafiri wa majini kwa wananchi wa Muleba Kaskazini hasa Vijiji jirani vya Kabale, Itoju, Izigo na Katoke; na kwa kuwa, hadi sasa hatuoni Mradi huo ukiendelea wala kupewa maelezo yoyote:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Gati la Kyamkwikwi?

(b) Je, kwa sasa litagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli katika bajeti za miaka ya 2004/2005 na 2005/2006, Wizara yangu ilikubali kujenga Gati la Kyamkwikwi. Katika mwaka wa fedha wa 2005/2006, ilitenga jumla ya shilingi milioni 150, kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa magati katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kutokana na ufinyu wa fedha, kiasi hicho hakikutolewa na Serikali kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa magati hayo.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara yangu ilikubaliwa tena na Bunge lako Tukufu, kutenga jumla ya shilingi milioni 150, kwa ajili ya ujenzi wa magati ya Kyamkwikwi, Bukondo, Maisome na Mwigobelo katika Ziwa Victoria, Karema katika Ziwa Tanganyika na ukarabati wa Gati la Kasanga katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, kiasi hiki cha fedha, hakitoshi kujenga magati sita na ukarabati wa gati moja. Kutokana na hali hiyo, Serikali iliona ni vema, fedha hizo kidogo zitumike katika kukarabati Gati la Kasanga ili kuliweka katika hali nzuri na ya usalama kwa meli, abiria na mizigo yao. Hata hivyo, kazi hii imechelewa kufanywa, kutokana na fedha zilizotengwa kwenye bajeti kuchelewa kutolewa. Hivi sasa maandalizi yanafanywa ili kazi ya ukarabati wa gati hilo, ianze chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Spika, gharama za ujenzi wa magari ni kubwa na Serikali haiwezi kujenga magati yote kwa wakati mmoja. Wizara yangu ikishirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania, itatoa kipaumbele katika ujenzi wa Gati la Kyamkwikwi katika mwaka wa fedha wa 2007/2008. Ujenzi wa Gati la Kyamkwikwi, unategemewa kuigharimu Serikali jumla ya shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mamlaka ya Bandari Tanzania, ina mipango ya kufanya utafiti wa bandari *(Ports Master Plan Study),* kubaini mahitaji muhimu katika bandari zake zote za Mwambao na Maziwa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwamba, ina mkakati wa kulijenga gati hilo kwa mwaka huu wa 2007. Lakini kwa miaka iliyotangulia, bajeti ilikuwa ni kidogo, shilingi milioni 150 kwa miaka miwili mfululizo hazikutolewa. Sasa Gati la Kyamkwikwi peke yake, limekisiwa kugharimu shilingi milioni 500.

Je, Wizara ya Fedha, inaweza ikatuhakikishia kwamba itaweza kututengea shilingi milioni 500 ili kuweza kujenga gati hili ambalo ni muhimu na ni kwa ajili ya usafiri katika Ziwa Victoria? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, mahitaji halisi ya nchi yetu katika mambo mbalimbali, yanaeleweka. Kama anakumbuka Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, *Lake Tanganyika* tuna magati 19, *Lake Nyasa* kuna magati zaidi ya 15 na *Lake Victoria* zaidi ya 20. Nafikiria Wizara ya Fedha kama itakuwa ina hali nzuri ya kifedha, inaweza ikatusaidia hela hiyo ya kujenga.

Lakini kwanza, tunachotakiwa kufanya ni kufanya *Ports Master Plan Study*, tuone hali halisi na mahitaji halisi na kuweka vipaumbele katika kufanya shughuli zetu za usafiri kwa kutumia magati.

Na. 5

**Matumizi ya Rada**

**MHE. BAKAR SHAMSI FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kupatikana kwa Rada ya kisasa ya Ulinzi na Usalama wa Anga ya Tanzania, kumechangia kuongezeka kwa mapato ya ada ya ndege zinazopita juu ya anga la nchi yetu, kutokana na uwezo wa Rada hiyo:-

(a) Je, ni mapato ya ziada kiasi gani yamepatikana tangu Rada hiyo ianze kutumika?

(b) Je, gharama za uendeshaji wa Rada hiyo kwa mwaka ni kiasi gani?

(c) Je, Rada hiyo imefanyiwa matengenezo mara ngapi na kwa gharama gani tangu ianze kutumika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Bakar Shamsi Faki, Mbunge wa Ole, napenda kwanza nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waongoza ndege hutumia Rada kuwezesha ndege nyingi kuruka kwa usalama na bila kugongana kwa wakati mmoja. Pia Rada hupunguza ucheleweshaji wa safari za ndege, kuwezesha kutelekezwa kwa ndege, kukwepa maeneo yenye hali mbaya ya hewa na husaidia marubani kuona uwanja wa ndege wa kutua.

Hata hivyo, Rada kama chombo kingine kinachotumika kuongoza ndege, hufanya kazi kwa kushirikiana na mitambo mingine kama ile ya mawasiliano na mitambo inayosaidia kuelekeza safari za ndege *(Navigational Aids).* Kwa hiyo, siyo rahisi kutathmini mapato ya ziada ambayo hupatikana kutokana na Rada peke yake. Mapato yote yanayohusika na urukaji kwenye anga *(Air Navigation Charges),* hujumlishwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Takwimu za mapato kwa kipindi cha miaka miwili kabla ya Rada kununuliwa ilikuwa kama ifuatavyo: Mwaka 2000/2001 - Sh.2,398,541,000.00 na Mwaka 2001/2002 - Sh.2,845,496,000.00. Baada ya Rada kununuliwa na kuanza kutumika, mapato yaliongezeka kama ifuatavyo: Mwaka 2002/2003 - Sh.3,408,821,000.00; Mwaka 2004/2005 - Sh.4,113,340,000.00; na Mwaka 2005/2006 - Sh.6,082,146,000.00.

Kwa hivyo, kumekuwepo na ongezeko la mapato kama nilivyoeleza, kutoka mwaka 2002 kabla Rada haijaanza kutumika hadi mwaka 2006. Ni dhahiri kwamba, ongezeko hili, kwa kiwango kikubwa, limetokana na kuongezeka kwa ndege, zinazotumia anga na viwanja vyetu kwa jinsi huduma zilivyoboreshwa na ongezeko la ukuaji wa utalii. Kuwepo kwa Rada, kumesaidia pia ongezeko hili, kwani wateja wetu wamekuwa na uhakika wa usalama zaidi wa ndege na abiria wake, wakati wanapita kwenye anga letu.

(b) Mheshimiwa Spika, wastani wa gharama za uendeshaji wa Rada kwa mwaka ni Sh.234,723,041.30 na mchanganuo ni kama ifuatavyo: Mishahara ya waongoza ndege na Wahandisi wa Rada Sh.145,597,121.30; mafunzo ya waongoza ndege na Wahandisi wa Rada Sh.50,000,000.00; matengenezo madogo madogo *(Routine Service)* Sh.6,704,330.00; matumizi ya umeme Sh.28,002,443.00; na usafiri wa wafanyakazi na matumizi mengine Sh.4,419,147.00.

(c) Tangu Rada hii inunuliwe, haijafanyiwa matengenezo makubwa. Hata hivyo, kulikuwa na utengenezaji wa *Uninterruptible Power Supply (UPS)* na ununuzi wa *batteries* mwaka 2006 na matengenezo ya *Motor* ya *Antenna* na jumla ya gharama ya vipuri na matengenezo hayo ilikuwa Sh.47,861,632.00.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa bei ya Rada hii imeleta utata na kwa kuwa Serikali ya Uingereza, pamoja na Serikali ya Tanzania, zinafanya uchunguzi; je, Waziri atakubaliana nami kwamba, kwa kuwa jambo hili limezungumzwa katika Bunge la Uingereza na katika Bunge letu, taarifa hiyo ya uchunguzi iletwe katika Bunge ili tujue ukweli wa tuhuma hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli na sisi tumesikia kwamba, bei ya Rada hii imeleta utata na shughuli hizi zinashughulikiwa, ninaamini aliyeunda Tume hiyo, ndiye

atakayepelekewa hiyo ripoti. Akiamua kuileta ripoti hiyo Bungeni, sisi tutashukuru, si tatizo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya Uingereza, imeamua kulichunguza suala hili; je, Serikali ya Tanzania itachunguza suala hili?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, tutashukuru, tunasubiri ripoti ya wenzetu Serikali ya Uingereza.

Na. 6

**Utekelezaji wa Mradi wa *Quick Start***

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ya mwaka 2002/2003, Waziri katika kulielezea Bunge utekelezaji wa ahadi za Wizara hiyo (uk. 6 - 9 wa hotuba hiyo), alizungumzia Mradi wa *Quick Start* na kwamba wananchi wa Wilaya husika, ikiwemo Wilaya ya Babati, watachangia Mradi huo wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Mwanzo na kuzikarabati nyingine zilizopo; na kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi kuwa nguvu za wananchi hazitapotea bure (uk. 9 wa hotuba):-

(a) Je, wananchi wa Wilaya ya Babati walichanga fedha kiasi gani kwa ajili ya Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mkoa?

(b) Je, fedha hizo zipo wapi na kama zipo zitatumika vipi ikiwa hatma ya mradi wa *quick Start* haijulikani?

(c) Je, Mradi huo ulikumbwa na matatizo yapi kwani ulipaswa kufadhiliwa na nchi wahisani na yale malengo yake yatatekelezwa vipi na Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo katika Wizara yangu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Babati, zinaonesha kuwa, Wilaya ya Babati, ilikusanya mchango na fedha zenye thamani ya shilingi milioni 28,738,500 kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama husika, ingawa lengo la awali lilikuwa ni kukusanya shilingi milioni 31,370,500.

(b) Taarifa zilizopo katika Wizara yangu zinaonesha kuwa fedha hizi zipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati na tayari mawasiliano kati ya Mahakama na Halamshauri ya Wilaya ya Babati, yameanza ili zitumike kama ilivyokusudiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Mradi huu wa *Quick Start*, uligharamiwa na wafadhili ambao ni Canada, Denmark, Finland, Netherlands, Norway na Sweden. Lakini Mradi huu ulifungwa baada ya muda wake kukamilika na kwamba, malengo ambayo hayakukamilika kwa utekelezaji, yameingizwa katika Mradi Mkubwa wa Maboresho ya Sekta ya Sheria, ambao unagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali na wafadhili mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo yaliyoukumba Mradi huu ni pamoja na gharama kubwa za ujenzi zilizowasilishwa, kuliko uwezo halisi wa Mradi. Kwa mfano, gharama za awali *(Preliminary Estimates)* za ujenzi wa Mahakama za Babati zilizowasilishwa, zilikuwa ni shilingi 1,444,000,000.00, kiasi ambacho kilikuwa kikubwa mno ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa kazi hiyo na hivyo kuamuliwa kuwa michoro ya ujenzi ibadilishwe ili iendane na bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', kwa kufuatilia kwa karibu, utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni ili kutatua matatizo na kero zinazowakabili wananchi wa Babati na pia wananchi wa Babati kwa kuwa na subira. Namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Babati, waendelee kuwa na subira wakati taratibu za utekelezaji wa malengo niliyoyataja hapo juu, zinafanyiwa kazi.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili:-

La kwanza, kwa kuwa gharama za ujenzi sasa zinazidi kupanda katika ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na Mkoa na ya Mwanzo kupitia Mradi huu. Je, Serikali sasa inasema nini kuhusu Mradi huu, umalizike mapema iwezekanavyo ili gharama zisiendelee kupanda kama alivyozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri?

La pili, kwa kuwa yapo malalamiko ya wananchi katika eneo ambalo linajengwa Mahakama kwamba, hawajafidiwa; Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakuwa tayari kufuatilia jambo hilo mapema iwezekanavyo ili waliotoa eneo hilo, waweze kupata fidia yao? Ahsante.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru na kumpongeza sana Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri ya msingi na vile vile napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali nayo ingependa kuona Mradi huu unakamilishwa upesi, kama alivyosema kwa maneno yake kwamba, gharama ya ujenzi isiongezeke.

Lakini kuhusu fidia kwa wale wananchi wa Babati, mimi nilifika kwenye eneo ambalo limepangwa kujenga Jengo la Mahakama ya Babati na ya Mkoa wa Manyara, kulikuwa hakuna mti wala nyumba na nilipofika Halmashauri ya Mji wa Babati, nilielezwa kwamba, fidia inayotakiwa ni shilingi milioni 70 na kwa maneno mengine basi, gharama ya ujenzi iongezeke na kwa hiyo, Serikali ianze kuchelewesha tena Mradi huu.

Baada ya kufuatilia kwa karibu sana, kwanza ni Halmashauri ya Wilaya ya Babati, ndiyo ambayo inapaswa kutoa eneo la kujenga Jengo la Mahakama na kwa hiyo, Halmashauri ilikubali kwamba, eneo lile litatolewa bure kama inavyofanywa kwenye maeneo mengine na hivyo suala la kufidia litakuwa la Halmashauri ya Wilaya ya Babati. Naomba Mheshimiwa Mbunge, asaidie kuona kwamba, fidia inayotakiwa na siyo ile ya shilingi milioni 70, inapatikana ili wananchi wasiendelee kulalamika.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Karatu ni mojawapo katika Mradi huu kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri; na kwa kuwa Mradi wa Karatu pia ulisimama; na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema tatizo ni gharama zimekuwa kubwa; je na mimi wa Karatu sasa nielewe kwamba, Mradi wa Karatu pia ulisimama kwa kuwa gharama zilikuwa ni kubwa?

Kama ni hivyo, kwa vile Mradi huu ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati ule; je, ni kweli Waziri anataka kuliambia Bunge hili kwamba, Mradi Mkubwa namna hii ulianzishwa bila kuwa na mpango kamili na kuwa na ramani inayojulikana na Serikali yenye bei halisi?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Quick Start* umesimama kwa sababu muda wake umefikia mwisho. Lakini makubaliano yetu ni kwamba, miradi yote ambayo ilikuwa inajengwa wakati ule, inahamishiwa sasa kwenda kwenye Mradi Mkubwa wa *Legal Sector Reform Programme*, ikiwemo pia Mradi huo wa Karatu.

Na. 7

**Mlundikano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA aliuliza:-**

Kwa kuwa kuna mlundikano mkubwa wa wafungwa na mahabusu magerezani: Je, kwa nini tusirudie utaratibu wa kuwa na wafungwa wa nje, ambao makosa yao si makubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, magereza yetu nchini hivi sasa yanakabiliwa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu. Kisheria Magereza yetu yanaruhusiwa kuhifadhi wahalifu 22,699, lakini yanakuwa na wastani wa wahalifu 45,000 kila siku.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwa na wafungwa wa nje, ambao makosa yao si mkubwa, bado upo na unaendelea kufanya kazi nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 38 cha Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, Mahakama imepewa uwezo wa kutoa adhabu ya kifungo cha nje, chenye masharti au kisichokuwa na masharti kwa kuzingatia aina ya kosa, uzito wa kosa na tabia ya mkosaji.

Mheshimiwa Spika, sanjari na adhabu ya kifungo cha nje, ili kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani, Bunge lako Tukufu, lilitunga Sheria ya *Parole*, ambapo wafungwa wenye vifungo virefu kuanzia miaka minne na kuendelea na wenye tabia njema, huweza kuachiliwa kwa mpango huu. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kati ya mwaka 2002 hadi mwaka 2006, jumla ya wafungwa 2,310 wameachiliwa huru chini ya Mpango huu wa *Parole.*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe, inaonekana kwamba idadi ya wafungwa ni 22,669, ndiyo kiwango cha kuweza kupokea lakini waliopo 45,000, maana yake ni zaidi ya nusu. Sasa Waziri anaweza akatueleza kwa idadi hiyo, wafungwa walio magerezani ambao makosa yao ni madogo ni kiasi gani?

Pili, Sheria ya *Parole* ilianza lini na utekelezaji wa kiwango hicho kwa wafungwa walioachiwa inalingana na utekelezaji wa Sheria?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, maswali mawili aliyouliza. Takwimu alizozieleza ni za kweli kabisa na ndivyo tulivyosema kwamba, tunao zaidi kidogo ya mara mbili ya wale ambao kwa mujibu wa Sheria, nafasi zinaruhusu. Sasa maswali yake ya kwamba, tutoe taarifa hapa, wafungwa wa makosa madogo madogo ambao wangeweza kutoka nje kwa njia ya *Parole* ni wangapi. Suala hili tunahitaji muda kwa sababu linatakiwa uchambuzi, tuweze kumjibu vizuri na kwa usahihi.

Napenda niseme kwamba, kwa taarifa ambazo ninazo, wale wafungwa wanaoweza kutoka kwa *Parole,* hawatoki wote kwa sababu inatakiwa Halmashauri za Wilaya na *DCs* wawe tayari kuwatumia. Sasa katika sehemu nyingine, Halmashauri za Wilaya wanasema hawana kazi za kuwapa. Lakini napenda nichukue nafasi hii, kuwahimiza Halmashauri za Wilaya na Wakuu wa Wilaya, kwa sababu wakati mwingine

wanakwenda kuwaajiri watu wanaowalipa mishahara mikubwa, wakati ambapo wangeweza kuwatumia hawa wa *Parole* ambao tuko nao. Kwa hiyo, naomba wawe na mawasiliano ya karibu na Wakuu wa Magereza, wajue namba ya wale ambao tayari wana-*qualify* kwa *Parole* ili waweze kuwatumia. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Takwimu za Serikali zimekuwa zinaonesha kwamba, mara nyingi mahabusu ni wengi kuliko wafungwa wenyewe. Kwa hiyo, ukitazama pengine kiini cha tatizo hili ni kuchelewa kwa upelelezi, pamoja na kupungua kwa Mahakimu. Mimi naiuliza Serikali ni lini basi wataweka utaratibu rasmi, utakaoshirikisha Wizara zote zinazohusika ili kuhakikisha kwamba, mahabusu wanashughulikiwa ikiwa ni Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara nyingine inayohusika? Naomba nisaidiwe ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kuhakikisha mahabusu wanatoka ili kuondoa huu mlundikano wa hao mahabusu ambao ni wengi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niziweke sawa takwimu, kwa sababu nikichukua wafungwa walioko Magerezani hadi mwishoni mwa mwezi Machi, tunao 42,832 na kati yao hao ni jumla ya walioko mahabusu, pamoja wafungwa. Kati yao wafungwa ni 22,622 na mahabusu ni 20,210. Kwa hiyo, kwa takwimu hizo, si kweli kwamba, mahabusu ni wengi kuliko wafungwa, isipokuwa napenda kukiri kwamba, idadi hiyo ya mahabusu ni kubwa kuliko ile ya kawaida na kuna haja ya kuchukua hatua mbalimbali, kupunguza jumla ya mahabusu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kupunguza idadi ya mahabusu, Serikali kupitia Idara zake za Mahakama, Polisi na Magereza, tunalishughulikia kwa bidii kubwa sana. Nakushukuru. *(Makofi)*

Na. 8

**Matangazo ya Dawa za Asili**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (k.n.y. MHE. JANETH B. KAHAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwepo na wimbi kubwa la matangazo ya dawa za asili, hususan zile za kuongeza kinga za mwili *(CD4)*, kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na zile za kuongeza nguvu za kiume:-

(a) Kwa kuzingatia kwamba, UKIMWI bado hauna dawa; je, Serikali ina habari na tiba hizo za asili na ufanisi wake ili kama haziongezi kinga ya mwili, wananchi wasiendelee kudanganyika na kuzidi kuzitumia huku wakiendelea kuathirika, hasa kwa kuzingatia kwamba tiba hizo siyo za wazi sana na pengine ni za gharama nafuu na kwamba zinafanya kazi vizuri, basi wahusika waombwe kuzisambaza kwa wananchi wengi kupitia kwenye Zahanati za Serikali?

(b) Je, Serikali inafahamu ni sababu gani zinasababisha kupungua kwa nguvu za kiume kunakotangazwa sana na waganga wa jadi?

(c) Je, tiba hizo za jadi za kuongeza nguvu za kiume, haziwezi kuathiri mfumo mzima wa kuzalisha, kwa kuzaa watoto wasio timilifu kimaumbile na akili?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo kuhusu tiba ya asili na UKIMWI:-

Tanzania ni moja ya nchi chache ulimwenguni, zenye uoto wa asili na kuwa na mimea mingi, yenye kuwa na uwezo wa kudhibiti virusi kwa ujumla wake. Mimea kama Mlonge, Mbaazi, Mzalia Nyuma (kwa Lugha ya Kizaramo) na Mbuyu, vina virutubisho vya mwili. Kutokana na mapokeo ya imani ya tiba za asili katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, waganga wa tiba asilia, wanaweza kuchanganya mchanganyiko wa mimea hiyo na mingine na ikamsaidia mgonjwa aliyeathirika na virusi, ikiwa ni pamoja na UKIMWI. *(Makofi)*

Hapa kwetu Tanzania, kuna vikundi vinavyojishughulisha na utoaji wa huduma kwa waathirika wa virusi vya UKIMWI, ikiwa ni pamoja na mtandao wa waganga wa tiba asilia, kikundi kisicho cha Kiserikali cha *Tanga AIDS Working Group (TAWG) na* Taasisi ya Tiba za Asili ya Muhimbili, ambapo Madaktari, Wanasosholojia na Waganga wa Jadi, wameungana na kufanya kazi pamoja na kutafiti na kutoa huduma kwa waathirika wa Ugonjwa wa UKIMWI, pamoja na kudhibiti magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina habari na tiba za asili zenye uwezo wa kuongeza tiba ya mwili na hasa kwa kudhibiti magonjwa nyemelezi. Serikali kwa kutambua hilo inaendelea kufanya tafiti za miti shamba hiyo. Hata hivyo, uwezo wa tafiti hizo bado haujawa wa kiwango kikubwa kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa kufanyia tafiti za kina za dawa na michanganyiko ya dawa zitumikazo na waganga wetu wa tiba asili. Ukizingatia kuwa tafiti huwa zinachukua muda mrefu, aidha, usiri wa waganga wa tiba asilia kuhusu dawa zao unakwamisha dhima za kutumia dawa hizo katika tafiti.

(b) Upungufu wa nguvu za kiume unasababishwa na mambo mengi, baadhi yao ni yale ambayo nitayataja pamoja na lishe duni hasa mboga za majani, kutokula aina mbalimbali za jamii ya karanga *(nuts)*, matumizi yasiyofaa ya ulevi kama pombe, sigara na dawa za kulevya, dawa zinazotibu baadhi ya magonjwa kama kisukari, shinikizo la damu, magonjwa ya akili na vilevile kutopumzika kunakosababishwa na shughuli nyingi za kijamii hivyo kusababisha uchovu.

(c) Dawa nyingi za tiba asili ni virutubisho ambavyo muhitaji angeweza kuvipata endapo angekula vyakula vyenye virutubisho hivyo. Pamoja na kuwa dawa hizo hazijafanyiwa utafiti wa sayansi ya leo na kutokana na unyeti wa usiri wa watumiaji wa dawa hizo zingekuwa na madhara zisingetumiwa na wananchi hata huko zinakotoka yaani maeneo yake ya asili. Hadi sasa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haijapokea taarifa ya tukio kutoka kwa walalamikaji wanaotumia dawa hizo za kuongeza nguvu za kiume.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nyawazwa sijui kwa nini unauliza hili naona zaidi linahusu zaidi wanaume, lakini una uhuru.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swala dogo la nyongeza, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika kuelezea dawa hizi za asili. Lakini Wabunge wa *TAPAC* walikuwa na semina tarehe 22 Machi, 2007 mpaka tarehe 24 Machi, 2007 katika kuangalia hali ya waathirika wa UKIMWI na kinga zake.

Mheshimiwa Spika, kiongozi wa waathirika alilalamika kwamba wanakunywa dawa hiyo sasa sijui leo hii Mheshimiwa Waziri aniambie ni dawa za asili au *CD4* wanamakalio yanakwisha na matatizo yanakuwa makubwa baada ya kunywa zile dawa. Je, Serikali inazijua dawa hizo, ni za asilia au ni za *CD4?*

La pili, je, kwa sababu maeneo ambayo sehemu za mwili ambazo waathirika wamelalamika kwamba wamekunywa dawa hizo makalio yamepungua ni sehemu mojawapo ya miili yao, wameathirika na matiti yamekuwa makubwa zaidi ya maumbile walivyopewa. Je, Serikali inawasaidie waathirika hao waliopatwa na maafa hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, naomba kusema kwamba dawa ambazo wamelalamikia, walilalamikia dawa hawakulalamikia suala la *CD4. CD4* ni kipimo ambacho kinaainisha ni kiasi gani mtu ameathirika. Kwa hiyo, dawa wanazolalamikia labda ni jibu swali linalohusiana na dawa sio kuhusu *CD4.*

Mheshimiwa Spika, dawa ambazo wanatumia tumepata taarifa ni kwamba walikuwa wanalalamikia dawa ambayo inaitwa *Entry 4* na 30 lakini bado sisi kama Wizara ya Afya tunafanyia uchunguzi kuweza kuona kama malalamiko yale kama kweli yanaletwa na zile dawa za *Entry 4* au nyingine zinatokana na hizi dawa kwa sababu wengi ambao wanakuja kutumia zile dawa za kurefusha maisha, zikiwemo hizo ambazo za asili na *Entry 4* ni kwamba wanalalamika kweli lakini hatuwezi kujua kwamba ametumia zile dawa peke yake kama *Entry 4* ambazo analalamikia au wamechanganya au kuna tatizo lingine. Sasa hivi Wizara ya afya kupitia *TFDA* na *NMRY* wanachunguza ili kuona kwamba tatizo liko wapi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ni kweli waliolalamika wanasema kwamba inaathiri baadhi ya sehemu zao za mwili ikiwa ni pamoja na makalio kuwa

yanapungua na matiti kuwa makubwa, sasa kusema kwamba Serikali itafidia kiasi gani, mimi nafikiri hilo suala watuachie kwanza tuone tatizo liko wapi, tusianze kusema tutalipa fidia kiasi gani wakati hatujajua tatizo lile limetokana na nini. Mimi naomba Waheshimiwa Wabunge muwe na subira Serikali inalifahamu hilo, tunafanya utafiti kuweza kuona tatizo liko wapi na ikipatikana tutatoa ushauri ili kuweza kuona hiyo hali inawezekana. Kwa hiyo, hatuwezi kusema tutatoa fidia wakati hatujui kwamba tatizo limetokana na nini.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa dawa za miti shamba hazina vipimo maalum na kwa kuwa katika awamu iliyopita Naibu Waziri wa Afya kama yeye alipokuwa anajibu swali linalolingana na hili aliwatia sana hamasa wanaume ili kuongeza nguvu watumie mti wa mbuyu na kwa kuwa baadhi ya wanaume hao waliotumia mti huo wa mbuyu bila kipimo chochote kwa hivyo nguvu zikaongezeka maradufu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje juu ya wale watu walioathirika kwa kuwa na nguvu za ziada?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba dawa hizi za asili ni mchanganyiko wa virutubisho na mchanganyiko wa virutubisho nikautaja ubuyu kwa sababu kule ndani kuna Vitamini C na kadhalika na vitu vingi na nimesema dawa za asili ambazo wanatumia huwa zinafanya mchanganyiko sasa kama huyo aliyetumia mbuyu mimi sidhani na kama imemsaidia kwamba yeye nguvu zake zimeongezeka, ushauri ambao ninaweza nikatoa ni kwamba dawa yoyote ile iwe dawa kama chakula, iwe dawa kama vidonge, huwa unapewa ushauri na yule anayekupa iwapo unaona dawa ile inakupa kama nguvu zinaongezeka, kama ni *side effect* ya dawa unayopewa.

Kwa hiyo, ushauri wangu mimi nashauri huyo aliyemwagiza aende kule kwenda kumuambia ili aweze kumpa vinginevyo jinsi gani atafanya ili aweze kukidhi tatizo lake hilo, kwa sababu kama siwezi nikamshauri kama yeye nguvu zake zimeongezeka kuliko alivyotarajia basi ni tatizo inabidi aende kwa mtaalam ili amshauri.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, napenda nichukue nafasi hii kama Serikali tuwaombe kabisa wananchi na jamii inayotusikiliza popote wanapokuwa na matatizo iwe kupungukiwa na nguvu za uume au matatizo mengine ya kiafya, mimi nawashauri waende kwa wataalam ili waweze kuwashauri vizuri, waweze kutumia dawa kutokana na maagizo badala ya kwenda tu kuchanganya na kutumia halafu baadaye huwezi kujua umeathirika kiasi gani.

Na. 9

**Dawa Zinazouzwa Kiholela**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina wajibu wa kuhakikiksha wananchi wake wanapata huduma nzuri za afya na dawa bora zilizo kwenye viwango vinavyokubalika:-

(a) Je, Serikali inaliangaliaje suala la dawa mbalimbali zinazotembezwa mitaani na kuuzwa kwenye mabasi?

(b) Kwa kuwa dawa yoyote inapotumiwa bila maelekezo ya kitaalam huweza kuwa sumu kwa mtumiaji na hivyo kuleta madhara kiafya na kwa kuwa wengi wanaotembeza na kuuza dawa hizo hawana taaluma yoyote ya kitabibu, je, Serikali haioni hatari kuwa wananchi wake watapata shida kiafya na hivyo kupoteza nguvu kazi ya Taifa letu?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka za kudhibiti biashara hiyo ambayo ilianza kidogo kidogo na sasa imeenea karibu mikoa yote?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na wauzaji wa dawa za binadamu hususan dawa za kienyeji zilizofungashwa kiufundi na hata zile za kitaalamu kutoka nchi za nje kama China katika baadhi ya mabasi yaendayo Bara kutokea Dar es Salaam na katika sehemu za mikusanyiko ya watu kama vile semina au warsha.

Tatizo hili linatokana na kujitokeza wafanyabiashara wasio waaminifu na wasiozingatia masharti ya uagizaji wa dawa nchini. Wafanyabiashara hao huingiza dawa hizi kwa kificho na hudiriki kuzificha kwenye bidhaa za kawaida kama vile sabuni au vifaa vya majumbani. Aidha, huwatumia vijana mbalimbali katika kuuza na kunadi dawa hizo katika mabasi na sehemu zenye mikusanyiko ya watu, kwa kutoa maelekezo kuhusiana na tiba ya dawa hizo ambao si sahihi. Mwenendo mzima wa biashara hii ni kinyume na matakwa ya sheria na chakula, dawa na vipodozi Na. 1 ya mwaka 2003.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli matumizi ya dawa kiholela bila ya kufuata maelekezo ya wataalam wa dawa ni hatari na yanaweza kusababisha madhara ya kiafya kwa mtumiaji na hivyo kupoteza nguvu kazi kwa Taifa letu. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa kufanya ukaguzi wa kufuatilia vyanzo vya dawa zisizoruhusiwa kisheria kwenye kliniki na maduka mbalimbali ya dawa. Kliniki na maduka yanayokutwa na dawa zisizoruhusiwa kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003 huchukuliwa na kuteketezwa.

Wizara imefanikiwa kuwakamata wauzaji wa dawa hizo katika mikoa ya Iringa na katika miji ya Kibaha, Pwani. Aidha, Mamlaka ya Dawa ilishatoa waraka kwa wamiliki

wote wa mabasi nchini, *Tanzania Bus Owners Association (TABOA)* kuwaagiza kutoruhusu wauzaji hao katika mabasi wanaomiliki kwani ni hatari kwa wateja wao.

(c) Katika kuhakikisha tunadhibiti tatizo hili Serikali kupitia Wizara yangu itaendelea kuwaelimisha wananchi kuacha kununua dawa zinazouzwa mikononi na vile vile kuwataka kutoa taarifa katika vyombo vya dola wanapoona wauza dawa kwenye mabasi ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Aidha, Wizara kwa kutumia vitengo vyake vinavyojihusisha na uelimishaji wa afya kama vile Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma na Mamlaka ya Chakula na Dawa itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya dawa. Kadhalika kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali Wizara itaendelea kufuatilia vyanzo vya dawa haramu na kuhakikisha kuwa vinadhibitiwa ili dawa hizo zisiweze kuwafikia wananchi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa biashara hii hufanyika wazi na hakuna usiri wowote hata sasa hivi ukitoka ukifika mjini utakuta wanauza hizo dawa mpaka sasa ningependa kujua kwamba ni wamiliki wangapi pamoja na wasambazaji wangapi wamechukuliwa hatua tangu Serikali itangaze kwamba hakuna kuuza dawa kiholela mitaani?

(b) Kwa kuwa kutokana na hali ngumu ya maisha wananchi wetu wanaona unafuu wa kupata dawa hizi katika njia za kiholela na kwa bei nafuu na hivyo inakuwa vigumu kwa wananchi hao kutoa taarifa wanapoona dawa hizo mitaani, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kutoa tangazo rasmi kuhusiana na kudhibiti biashara hii ikiwepo kupiga marufuku kabisa na kuchukua hatua za uhakika na za kudhibiti biashara hii pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu wale ambao wanakiuka tangazo hili baada ya Serikali kutangaza rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Serikali inakiri kwamba hizi dawa zinauzwa wazi na kwamba hakuna usiri lakini naomba kusema kwamba siwezi sasa hivi nikatamka kwamba ni wangapi kwa idadi. Mimi nafikiri ni bora mimi tuwasiliane naye na nitaweza kumpatia hizo *data* kwa sababu ni mahesabu na sipendi niseme hapa uongo, nitampa kitu kizuri, tuwasiliane ili tuweze kumpa hiyo idadi. Lakini nahakikisha kwamba hao watu wapo wameshikwa na tunawafahamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Mbunge kusema kwamba wananchi kwa sababu ya maisha duni na kuuzwa kiholela, kwa maana hiyo wanakwenda kununua hizo dawa, mimi napenda nisikubaliane naye. Serikali yetu ina vituo vya afya, ina sehemu za kutolea huduma za afya na huduma ni bure na zipo. Katika sehemu kubwa dawa inapatikana na si hivyo tu, mbali ya vituo ya kutolea huduma vya afya vya Serikali bado kuna vituo vinatoa vipimo vya mashirika ya dini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachoomba hapa, wakati sisi tunatoa elimu kwa umma na kwa jamii, tunaomba tushirikiane. Kama kweli watu wanaweza kuona kwamba kuna umuhimu wa kwenda hospitalini kuwaona wataalam waweze kupatiwa huduma hizi mimi sioni kwa sababu gani mtu aende kiholela. Kuwa na kutokuwa na fedha mimi sioni kama ni kigezo cha kumfanya mtu atumie dawa kiholela ambayo tayari ameshaambiwa kwamba inamhatarishia maisha yake.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuendelea kusisitiza na kuwaambia wananchi hairuhusiwi kutumia, wale wanaouza kiholela wanafanya kosa, lakini vilevile wananchi tunaomba tushirkiane. Ninyi ndio mnaonunua na ndio mnaoendekeza hao watu. Kwa hiyo, mimi naomba wazidi kwenda hospitalini wapate maelekezo na wataalam wa afya ili waweze kupata dawa, dawa zipo ambazo zina bei rahisi, Serikali inatoa pesa nyingi sana kwa kununua dawa, kwa hiyo, wananchi watumie fursa hii kwenda kupata tiba sahihi katika vituo vya afya.

Na. 10

**Mafunzo ya Kilimo cha Kahawa**

**MHE. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Kwa kuwa taasisi ya *TACRI* imekuwa ikitoa mafunzo ya kilimo bora na cha kisasa cha Kahawa mpya na ile ya zamani kwa wakulima na baadhi ya wakulima hao wameweza kufuzu vizuri na kuwa walimu wa wakulima wenzao:-

Je, Serikali ipo tayari kusaidiana na *TACRI* ili kuwafundisha wakulima wengi zaidi na kuwapa motisha hao walimu wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania *(Tanzania Coffee Research Institute (TACRI)* hutoa mafunzo ya kilimo bora cha kahawa kwa wakulima nchini. Mwaka 2004/2005 hadi sasa, wakulima 2,250 kutoka Wilaya 20 wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha kahawa kupitia vituo vya Lyamungu (Hai), Mbinga (Mbozi), Maruku (Bukoba) na Ugano (Mbinga). Wakulima 170 kutoka Wilaya ya Hai wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha kahawa.

Aidha, Serikali inatumia njia mbalimbali kutoa motisha kwa wakulima walimu ikiwa ni pamoja na safari za mafunzo nchini na kubadilishana uzoefu na wenzao. Kwa mfano, katika mwaka 2005/2006 Halmashauri ya Wilaya ya Hai iliwezesha wakulima walimu nane kufanya ziara ya mafunzo Wilayani Mbinga, Mkoa wa Ruvuma.

Kwa kutambua umuhimu wa wakulima walimu, Wizara imekwishatoa mwongozo kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini jinsi ya kuendesha na kusimamia mafunzo ya wakulima walimu na kuwa na mfumo endelevu wa wakulima hao.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kusisitiza kuwa Halmashauri za Wilaya ndiyo waajiri wa Maafisa Ugani ambao wanapeleka ushauri na mafunzo kwa wakulima. Kwa hiyo, ni muhimu Halmashauri za Wilaya zizingatie eneo hilo katika mipango yao ya maendeleo ya kilimo *(DADPs).* Hii ni pamoja na kubuni utaratibu wa kutoa motisha kwa wakulima walimu.

Aidha, Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa *TACRI* na taasisi nyingine zinazotoa mafunzo kwa wakulima kwa kuwajengea mazingira mazuri ya utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kuielekeza *TACRI* fursa za fedha zilizopo na zinazoweza kutumika kuendeleza zao la kahawa.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, ningependa nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa kilifanyika kikao maalum kwa kuitishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ile mikoa inayolima mazao makuu ya biashara, zao la kahawa likiwa ni mojawapo na kuwekeana malengo ya kuzalisha tani 120,000 ifikapo mwaka 2010; je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza hivi vituo kwa ajili ya kuzalisha miche mingi zaidi ya kahawa kwa maana ya kuwa na bustani mama ili kuhakikisha pia kila kijiji kinaweza kupata bustani ya miche ili iweze kuwafikia wakulima kwa wingi zaidi na kwa mfano katika kuongeza hivi vituo vya bustani mama katika maeneo mapya zaidi, kwa mfano Rungwe, kule Kigoma pamoja na maeneo mengineyo ambayo yanalima kahawa kwa hivi sasa?

(b) Nashukuru Serikali pia imeona umuhimu wa walimu wakulima, je, hawa wakulima wa walimu isingefaa wakapatiwa vyombo vya usafiri kwa mfano pikipiki ili waweze kuwafikia wakulima wenzao kwa urahisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaona umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa kahawa na hasa baada ya mkutano ule wa wadau wa kahawa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulikubaliana kwamba lazima tutoke kwenye uzalishaji wa sasa wa tani 45,000 mpaka tani 120,000 ifikapo mwaka 2010 na ndio maana basi tumechukua jukumu la kuhakikisha kwamba uzalishaji wa kahawa unaongezwa na hasa kwa kutafiti miche mipya hii ambayo inazalishwa kwa njia mbalimbali za kitaalam ikiwa ni pamoja na kuzalisha vikonyo kwa sababu miche hii sasa ina ukingani mkubwa wa magonjwa yale ya *CBD* na kutu ya majani.

Sasa tunachokifanya sasa hivi ni kuiambia au kuisaidia *TACRI* kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kuionyesha fursa zilizopo katika miradi iliyopo kama ile miradi *DADPs* kwa wilaya zenye *DADPs* katika programu ya *SDP* ili waweze kupata fedha zile kuanzisha vituo mbalimbali katika Tanzania. Kwa kweli si rahisi ni kazi

kubwa, lakini hivi sasa napenda niwafahamishe Wabunge tayari *TACRI* imeshaanza kuanzisha vituo katika mikoa mbalimbali kulingana na fedha zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna kituo kidogo kimeanzishwa kule mkoa wa Kigoma wamepewa nafasi katika kijiji cha mwayaya na wamejenga na wamepeleka mtaalamu tayari, na vipo vituo vingine viwili pia sikumbuki ni vituo gani lakini navyo pia vipo mbio kuanzishwa katika mikoa mingine. Kwa hiyo huo ndio utaratibu ambao tunaufanya kuhusu kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakulima walimu, suala la kuwapa pikipiki mimi nadhani sasa hivi si muda wake kwa sababu kwanza mabwana shamba wetu wenyewe, wale ambao tumewaajiri bado hatujawapa hata baiskeli za kuwatosha. Tunasema tunawatafutia vitendea kazi na hawa wakulima walimu kwa sehemu kubwa tunataka wafundishe kwa kutumia mashamba darasa, yaani tukishapata nyezo wale wakulima wako huko huko ndani ya mashamba yale, kwa hiyo, mashamba yao ndiyo madarasa kwa hiyo hakutakuwa na sababu ya kutafuta fedha za kuwanunulia pikipiki.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mpango huu ambao umeandaliwa na taasisi ya utafiti ya *TACRI* umeleta mafanikio kwa kufikisha taaluma ya kilimo kwa wakulima walio wengi na kwa tatizo hili la elimu ya wakulima kwa mazao mbalimbali ni kubwa kutokana na uhaba wa maafisa wa ugani; je, Serikali au Wizara itakubali kuanzisha mpango huu kwa mazao tofauti ili elimu kwa wakulima iweze kuwafikia wakulima walio wengi popote walipo kwa kuchukua mfano wa mafanikio ya taasisi hii ya *TACRI?*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mafanikio haya yaliyoonyeshwa na *TACRI* ni mfano halisi yaani ni *mode of application* ambayo tungependa tuyatumie hata kwa mazao mengine.

Na. 11

**Mazao yanayotoa *Bio-Diesel***

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE** aliuliza:-

Kwa kuwa hali ya upandaji wa bei ya mafuta ya petroli mara kwa mara inadhoofisha maisha ya Watanzania walio wengi kutokana na sababu kuwa upandaji huo wa mafuta husababisha pia upandaji wa bei za bidhaa na huduma mbalimbali nchini na kwa kuwa imegundulika kuwa yapo mazao ya kilimo ambayo yanaweza kutoa mafuta ya petroli:-

(a) Je, ni mazao gani ya kilimo yanayotoa *bio-diesel?*

(b) Je, kati ya mazao hayo ni mazao gani yanayoongoza ki-asilimia kwa kuwa na mafuta hayo?

(c) Je, ni kwa kiasi gani Serikali imehamasisha wananchi kulima mazao hayo?

**SPIKA:** Kuna kasoro kuhusu namba Mheshimiwa Naibu Waziri, ni namba 11 tu ilikuwa ni namba ya awali, kwa hiyo, lijibiwe swali namba kumi na moja la Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, atuwie radhi kwa hizi kasoro za kuandika. Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli pamoja na athari za mafuta hayo katika mazingira kumewezesha vyanzo vya nishati inayotokana na mimea kugunduliwa. Vyanzo hivyo ni *bio-fuels* ambayo inaweza kuwa *bioethanol,* nishati mbadala ya petroli au *bio-diesel*, nishati mbadala ya dizeli.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mazao ya kilimo yanayotoa *bio-diesel* ni pamoja na Jatropha, Michikichi, Alizeti, Korosho, Nazi, Mbegu za Pamba na Ufuta. Mazao haya ni yale ya jamii ya mbegu za mafuta.

(b) Mazao yanayoongoza kiasilimia kwa kutoa mafuta ya *bio-diesel* ni pamoja na nazi asilimia 65, karanga asilimia 45 hadi 55, Korosho asilimia 46, Michikichi asilimia 43 hadi 51, Alizeti asilimia 25 hadi 85 na Jatropha yaani Mibono asilimia 33 hadi 60.

(c) Kwa kutambua fursa kubwa zilizopo nchini kwa kilimo cha mazao ya nishati mbadala Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuhamasisha sekta binafsi ya sukari kuongeza uzalishaji wa miwa kwa lengo la kutumia miwa hiyo kuzalisha sukari na *bioethanol.* Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa imepanga kupanda jumla ya hekta 600 za Jatropha kwa lengo la kuzalisha mbegu zitakazosambazwa kwa wananchi ili kuzalisha zao hilo kuanzia msimu wa mwaka 2009/2010.

(ii) Wizara imekuwa ikiwasaidia wawekezaji mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuendeleza mazao ya nishati nchini mwaka 2002/2003. Jumla ya

makampuni 11 yamewekeza katika kilimo cha mazao ya *bio-fuel* nchini yakiwemo makampuni ya *FELISA* mkoani Kigoma, *AMMA* ya Mkoani Tanga, *Diligent Tanzania Ltd.*, iliyopo Arusha, *PROCON* na *DIADEM* zilizopo Rukwa na *CEPA* iliyopo Mkoa wa Morogoro. Aidha, jumla ya makampuni 18 yamejiandikisha kuwekeza katika kilimo cha *biofuel* nchini.

(iii) Wizara inaendelea kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima wakufunzi kuhusu kilimo bora cha Jatropha. Katika msimu wa mwaka 2005/2006 jumla ya wataalam 15 kutoka mikoa ya Tanga, Arusha, Mbeya, Pwani, Morogoro, Dodoma, Dar es Salaam na Ruvuma walipatiwa mafunzo maalum ya kilimo bora cha Jatropha juu ya ukamuaji wa mbegu na matumizi ya mafuta hayo kutengeneza sabuni.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEHE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa na swali moja tu la nyongeza aweze kutuwekea sawa, je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuweza kuhamasisha upatikanaji wa teknolojia ya ukamuaji wa mafuta kutoka mazao hayo ndani humo humo nchini, ili bei ya mafuta iweze kuwa nafuu kuliko kuuza mazao haya kama malighafi katika viwanda vya nchi za nje kitu ambacho itasababisha tena bei ya mafuta iwe kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Serikali tayari imekwishaweka mikakati ya kuhakikisha kwamba uzalishaji wa mazao haya yanayotoa mafuta unashughulikiwa, ikiwa ni pamoja na kuunda sekretarieti katika Serikali ambayo itasimamia uendelezaji wa mazao haya kuwahamasisha wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuzalisha pamoja na kukamua mazao haya.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa kuanzia tu huko Arusha tayari tunayo *NGO* ambayo inajulikana kwa jina la KAKUTE, hii ni Kampuni ya Kueneza Teknolojia ndio maana inaitwa KAKUTE na mojawapo ya mambo ambayo wanatusaidia katika hili ni kuhakikisha kwamba mbegu za mazao haya zinapatikana na kusambazwa lakini pia wananchi wanafundishwa namna ya kuyakamua mafuta haya ndio maana mahali pengine tayari wanatengeneza sabuni na kule Arusha nimeona pia watu wengine wanatumia mafuta haya haya katika koroboi zao. Kwa hiyo, Serikali inafanya juhudi katika kueneza teknolojia hiyo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa tani 500,000 za muhogo zinaweza kutupa lita 200,000 za petroli na umeme kama megawati mbili na kwa kuwa taarifa hizi tayari zilishafikishwa Serikalini; na kwa kuwa Mikoa ya Kusini inazalisha muhogo wastani wa tani 5,000,000 kwa mwaka; je, Waziri haoni matatizo ya umeme na mafuta yaliyopo Kusini yangeweza kutatuliwa kwa njia hii wakati teknolojia yenyewe tayari ipo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mazao haya yapo katika makundi mbalimbali ya kuzalisha nishati, yapo mazao yanayotokana na *starch* kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, yapo mazao yanayotokana na mazao ya sukari kama miwa inayotoa *ethanol,* yapo hii jamii ya mbegu za mafuta kama Michikichi na Jetrofa inayotoa *bio-diesel* na hata mazao mengine kama Mananasi na Mtama mweupe ambao una *starch,* yote hayo yana viwango tofauti tofauti vya kuzalisha nishati na hata Soya inazalisha nishati kwa kiwango fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba mazao yote haya yanayoweza kutoa nishati yanashughulikiwa na ndio maana Serikali imeunda sekretarieti ambayo inatazama ni jinsi gani tunaweza kuzalisha *bio-diesel, ethanol* katika nchi hii ili tuweze kutumia mazao yetu kama tunayo. Kwa hiyo, hata mikoa ile inayozalisha muhogo tutaipa kipaumbele.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea! Kwa sababu tulianza na shughuli za kiapo zilizochukua muda katika maswali nimeshauriwa hapa kwamba tunaweza kuendelea kidogo ili tuyapunguze maswali. Swali linalofuata linaelekezwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi linaulizwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa niaba ya Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

Na. 12

**Elimu kwa Walemavu**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k.n.y MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA)** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini Serikali imewanyima walemavu fursa ya kusoma bure ngazi zote?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fursa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako naomba nitoe shukrani za dhati kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Stella Manyanya, kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa agizo lake na ushirikiano mkubwa alioutoa katika uhamasishaji wa ujenzi wa shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niwashukuru kwa dhati kabisa Naibu Mawaziri ambao walifanya ziara ya ukaguzi na uhamasishaji, kazi ambayo wameifanya kwa maarifa na juhudi kubwa na imeleta mafanikio makubwa sana ya kujivunia.

Baada ya hapo naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Serikali inasisitiza kutoa elimu kwa raia wake wote kama haki ya msingi bila kubagua rangi, kabila au maumbile. Kwa kuzingatia sera hiyo, watoto wote bila kubagua wanaandikishwa na kusoma bure katika Shule zote za Msingi za Serikali.

Aidha, Serikali inao utaratibu wa kuwagharamia Elimu ya Sekondari wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato duni ambao wamefaulu mtihani wa Darasa la Saba na kupata nafasi katika Shule za Sekondari za Serikali. Hivi sasa kuna jumla ya wanafunzi 45,000 wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne wanaogharamiwa na Serikali wakiwemo wanafunzi wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali hugharamia elimu ya wanafunzi hao baada ya kupokea orodha ya majina kutoka kwenye Halmashauri zao za Wilaya. Serikali itaendelea kuongeza huduma hii kwa wanafunzi wengi zaidi wa aina hii kadri ya uwezo wa fedha utakavyoruhusu. Aidha, tunaziomba Halmashauri za Wilaya nazo ziendelee kuongeza nguvu ili kuweza kugharamia elimu kwa wanafunzi wengi wa aina hiyo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali kweli imeonyesha juhudi ya ziada kabisa katika kuhakikisha inawalipia ada baadhi ya wanafunzi hao wenye ulemavu kwenye shule mbalimbali hapa nchini, lakini shule hizo zimekuwa zikikabiliana na matatizo makubwa ya vifaa vya kuwahudumia wanafunzi hao wenye ulemavu kwa namna moja au nyingine; je, Serikali sasa itaona umuhimu wa kutenga pesa au bajeti maalum ya kukarabati au kununua vifaa vipya vinavyoendana na mahitaji ya wanafunzi hao wenye ulemavu katika maeneo hayo wanayosoma?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba kwa kuwa elimu yoyote inaanzia na elimu ya msingi kama ndicho chombo hasa cha kuwajenga wanafunzi na tumekuwa na shule nyingi za ulemavu za msingi katika nchi yetu ambayo kwa kweli mazingira yake yameshakuwa katika hali mbaya kwa kuzingatia umuhimu huo huo wa kuwasaidia wanafunzi na watoto wenye ulemavu;

Je, Serikali iko tayari sasa kuandaa pia mpango maalum wa kuzikarabati na kuzihudumia ipasavyo shule za wanafunzi wenye ulemavu na hasa zile za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tunajitahidi kutoa vifaa na kufanya ukarabati, kwa mfano, shule za msingi za walemavu zipo chini ya Wizara ya Serikali za Mitaa na wanaendelea kutoa vifaa. Katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 walemavu walitengewa fedha na shule kadhaa zimefanyiwa ukarabati na mojawapo iko Mbulu, Basuto na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza vifaa ambavyo vitaweza kuwapatia uwezo zaidi, naomba niseme Wizara yangu imekuwa ikiwapatia vifaa wale wanafunzi waliopo kwenye hizi shule maalum ambazo ni pamoja na vifaa vya kuweza kupata uwezo mkubwa wa kusikia, zipo mashine za kuandikia *Braille* na pia wanafunzi ambao wana ulemavu wa viungo wameweza kupatiwa baiskeli, viti na wale ambao ulemavu wao unahitaji kupatiwa magongo pia wamepatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba niseme Wizara yangu imeipatia kipaumbele Idara hiyo ambayo kwa kweli tunaona idadi ya wanafunzi walemavu inaongezeka na sisi tutajipanga vizuri kwa kadri bajeti itakavyoturuhusu.

Na. 13

**Matatizo Yanayoikabili *NECTA***

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo matatizo yanayoikabili *NECTA* katika uendeshaji na usimamiaji wa Mitihani ya Taifa kama vile usimamizi duni wakati wa kufanya mitihani, usajili wa watahiniwa bandia wa kujitegemea na ucheleweshaji wa ada za usajili wa watahiniwa kutoka shuleni, vyuoni na kwa wazazi:-

(a) Je, Serikali inayatatua vipi matatizo hayo?

(b) Je, Baraza la Mitihani linaathirika vipi na matatizo hayo?

(c) Je, ni hatua gani za kisheria zinachukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa yapo matatizo yanayolikabili Baraza la Mitihani la Tanzania yakiwemo ya uendeshaji na usimamiaji wa Mitihani ya Taifa, usajili wa watahiniwa bandia wa kujitegemea na ucheleweshaji wa ada za usajili kutoka shuleni, vyuoni na kwa wazazi. Serikali katika kutatua matatizo hayo imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuhakikisha kuwa wasimamizi wa mitihani hawatoki katika shule wanazosimamia mitihani;

(ii) Kutoa semina na maelekezo ya kutosha kwa wasimamizi wote kabla ya mtihani kufanyika;

(iii) Kuwachukulia hatua za kinidhamu na za kisheria wasimamizi wote wanaobainika kukiuka taratibu za uendeshaji wa mitihani;

(iv) Kuhakikisha kuwa Watahiniwa wanapojisajili kufanya mtihani wanaleta picha mbili ambazo hutumika kama kitambulisho cha kumruhusu mtahiniwa kuingia kwenye chumba cha mtihani. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha mfumo wa usajili na utoaji wa matokeo ya mitihani ili kuziba mianya ya kuwepo na watahiniwa bandia wa kujitegemea.

(v) Kutoa Waraka wa Elimu Na. 9 wa mwaka 2002 unaowataka Wakuu wa Shule kuwasilisha ada za mitihani kwa wakati.

(b) Mheshimiwa Spika, matatizo ya uchelewaji wa ada ya mitihani yanaliathiri Baraza la Mitihani katika maandalizi ya mitihani, kwani lengo la kutoza ada ni kuwafanya watahiniwa wachangie gharama za uendeshaji mitihani. Aidha, usimamizi duni wa mitihani na usajili wa watahiniwa bandia husababisha udanganyifu katika mitihani. Hali hiyo hulifanya Baraza la Mitihani kutumia muda mwingi na kuingia gharama za kufanya uchunguzi inapobainika kuna dalili za udanganyifu. Aidha, udanganyifu katika mitihani una athari kubwa kwa Baraza na Taifa kwa ujumla kwa sababu kufanya hivyo ni kuhujumu elimu ya nchi.

(c) Mheshimiwa Spika, hatua za kisheria zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na matatizo hayo ni pamoja na;

(i) Kuwafutia matokeo ya mitihani watahiniwa wote wanaothibitika kufanya udanganyifu;

(ii) Watahiniwa wa shule/vyuo wanaochelewa kulipa ada huzuiliwa matokeo yao hadi hapo watakapolipa ada wanayodaiwa. Watahiniwa wa kujitegemea hawasajiliwi kufanya mitihani bila kulipa ada.

(iii) Kwa upande wa wasimamizi hatua za kinidhamu huchukuliwa kama vile kuvuliwa madaraka, kutoruhusiwa kushiriki katika shughuli za Mitihani ya Taifa na kufikishwa kwenye vyombo vya dola kwa hatua za kisheria; na

(iv) Watahiniwa bandia wanaobainika hufikishwa kwenye vyombo vya dola ambapo hushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

(a) Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa wanatoa waraka ili kuhakikisha kuwa ada zinafika kwa wakati, lakini baadhi ya Walimu Wakuu wa Shule wanachelewesha ada hizo na *progress* za wanafunzi kwa wakati.

Je, walimu kama wale ambao wanachelewesha wanachukuliwa hatua gani baada ya kuadhibiwa wanafunzi?

(b) Kwa kuwa wakati mwingine Baraza la Mitihani linakabaliwa na tatizo la fedha kuhusu usafirishaji na posho za walinzi; je, Wizara inalisaidiaje Baraza hili wakati ambapo inafikia hatua ya kusafirisha mitihani?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuhusu adhabu wanayopewa wanaochelewesha kupeleka ada za wanafunzi, naomba nikiri kwamba wamekuwa wakipata makaripio makali na baadhi yao ambao wamefanya hivyo pale ambapo inabainika fedha zile wamezitumia visivyo hatua za kisheria huchukuliwa kuwakabidhi kwenye vyombo vya dola.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu posho ya watumishi wanaofanya kazi za mitihani naomba niseme kwamba suala hilo limeletewa mapendekezo na Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inalifanyia kazi. *Inshallah* katika kipindi cha bajeti kijacho huenda kukawa na mabadiliko

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa wakati wa maswali naona nimeongeza lakini bado mambo yanaendelea maswali mawili yaliyobaki yataendelea kuulizwa kesho au siku inayofuata, namwita Katibu kwa shughuli inayofuata.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 41 ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 41 ya Bunge la Jamhuri ya Muungano inahusu masuala yanayohusu Haki za Bunge. Kanuni husika inasema kama ifuatavyo, naomba nisome: “Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na Haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mfululizo wa shughuli uliowekwa na Kanuni ya 23(4) na atakuwa amemuarifu Spika mapema kuhusu kusudi lake hilo na jambo ambalo anataka kuliwasilisha.”

Mheshimiwa Spika, naomba pia nisome Kanuni ya 41(4) ambayo inasema kwamba: “Mambo yanayohusu Haki za Bunge yatawasilishwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa katika Kanuni ya 23(4) lakini endapo wakati wa kikao chochote cha Bunge jambo lolote litazuka ghafla ambalo linaonekana kama linahusu Haki za Bunge

isipokuwa tu wakati huo kura inapigwa shughuli zitasimamishwa kwa madhumuni ya kuliwezesha jambo hili kuwasilishwa na kuamuliwa."

Mheshimiwa Spika, nimewasilisha mbele ya ofisi yako suala linalohusiana na Kanuni ya 41, ninaamini umepata. Kwa kuzingatia kwamba hii Kanuni ya 41(4) ambayo nimeisoma hapa ambayo inaruhusu suala kujadiliwa hata kama halijawekwa katika programu za Bunge siku hiyo ilimradi tu watoe katika kipindi cha kupiga kura, nilikuwa naomba mwongozo wako kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Haroub Said Masoud, nawaelewa kwa sababu najua mambo yanayoendelea, suala ambalo linatarajiwa kuletwa na Mheshimiwa Halima Mdee ni suala ambalo leo asubuhi hii kabla hatujaondoka humu nitalitolea uamuzi. Kwa hiyo, ningeona hakuna haja yoyote ya kuendelea na majadiliano yoyote kuhusu suala hili kwa sababu Spika atatoa uamuzi. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

(i) Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa mwaka 2007 *(The Supplementary Appropriation Bill, 2007);*

(ii) Muswada wa Sheria ya Kusimamia Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho kuona wa Mwaka 2007 *(The Optimetry Bill, 2007);*

(iii) Muswada wa Sheria ya Barabara wa mwaka 2007 *(The Roads Bill, 2007);* na

(iv) Muswada wa Sheria ya Wataalam wa Maabara za Afya wa mwaka 2007 *(The Health Laboratory Practitioners Bill, 2007).*

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura ameniomba nitambulishe wageni wake waliomsindikiza kwa kuja kuapishwa. Kwanza ni ndugu Saidi Wale anayetoka *Mafinga Secondary School* naomba asimame, ndugu Asha Wale ambaye anatoka Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam, Mheshimiwa hakusema uhusiano wake na hao lakini nadhani ni mashabiki wake. *(Makofi)*

Ndugu Leseng'waa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Dodoma, Ndugu Lusinde, Kada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Kongwa na Ndugu Siwa ambaye Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura anasema ni rafiki yake wa karibu sana hapa Dodoma. *(Makofi)*

Navutiwa kwamba Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura anaonyesha hana ukabila, marafiki zake na watu wanaomsindikiza wametoka katika mikoa mbalimbali na ni dalili nzuri sana na unaonyesha mwanzo mzuri. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nasikitika kuwataarifu kwamba wenzetu wanne walikumbwa na tatizo la kuvamiwa na majambazi mwezi uliopita nao ni Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha katika barabara ya Kibiti - Lindi kuelekea Ikwiriri, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Savelina Mwijage na Mheshiwa Shoka Khamis Juma.

Kwa niaba yenu nilishawapa pole kwa tukio hilo ambalo lilikuwa la hatari sana na ninakumbuka Mheshimiwa Shoka Khamis Juma alipokuja kuniona ilikuwa jicho limeziba na jekundu kabisa, samahani Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha ndio aliumizwa vibaya zaidi kuliko wengine. Kwa sababu walinyang'anywa kila kitu, kwa niaba yenu, Ofisi ya Bunge nilichukua uamuzi ya kuwapa ruzuku ndogo tu ya shilingi 250,000/= kila mmoja ili angalau wafike nyumbani kwao na kuweza kufunga mizigo kuja safarini Dodoma, poleni.

Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe na Mwalimu Msaidizi wa *Bunge Sports Club* anapenda kututangazia sisi wote Wabunge kwamba mazoezi ya viungo yataanza kesho Jumatano kama kawaida saa 11.30 asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, mara baada ya kipindi hiki cha maswali tunaombwa kwa haraka kadri inavyowezekana tuende tukapate *briefing.* Kama mnavyojua ilitakiwa tutangulie na *briefing* siku ya jana kama ilivyo kawaida kabla ya Mkutano kuanza, lakini kwa kuwa jana ilikuwa ni sikukuu basi uongozi wa Bunge uliona ni vizuri leo tuahirishe baada ya kipindi cha Maswali tupate *briefing* na kwa mtiririko ufuatao tuendelee na shughuli kama ifuatavyo, baada ya *briefing* tutakuwa na kipindi kifupi sana cha *lunch break* kama saa moja tu na saa 8.00 mchana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ataendesha semina fupi ya *Power Point Presentation* pale ukumbi wa Msekwa kule kule tutakapofanyia *briefing* na semina hiyo haitarajiwi kuchukua zaidi ya saa 1.30.

Baada ya hapo saa 10.00 jioni Wabunge katika vyama vyenu sasa mtakaa katika vyama *caucus* ili kuzingatia kama kawaida utaratibu wa shughuli zilizo mbele yetu, wale wa CCM kwa sababu ya idadi yao watabaki kwenye ukumbi ule ule wa Msekwa au watarudi kwenye ukumbi wa Msekwa na ofisi imeandaa utaratibu wa kawaida kwa wale wa vyama wa vingine.

Waheshimiwa nimeombwa nitangaze kwamba sasa kwa tangazo hilo ambalo nimekwishaletewa linasema kikao cha Wabunge wote wa CCM saa kumi jioni ukumbi wa Pius Msekwa nimeshatangaza. Lakini kabla ya hapo kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi wa CCM *caucus* saa tisa alasiri, kwa hiyo, wakati semina inamalizika basi wale wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa CCM *caucus* watakutana katika ukumbi wetu wa kawaida karibu na Ofisi ya Spika.

Waheshimiwa Wajumbe, nilipokea chini ya Kanuni ya 41 ombi la Mheshimiwa Halima Mdee kuhusu Haki za Bunge, akieleza humo amesoma sasa hivi asubuhi jinsi ambavyo anadhani yeye Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Adam Malima alivyoathiri sifa ya Bunge, sifa ya Spika na ina maneno na maelezo, sasa mimi nimeomba nikatae isisomwe na ninazo sababu naomba niwaeleze.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili la Mheshimiwa Adam Malima sasa hivi linaanza kuchukua sura ambayo italifanya Bunge letu liwe ni Bunge la kuchekwa. Nasema hivyo kwa sababu kilichokuwepo mbele yetu ni uamuzi wa Spika kwamba Mheshimiwa Adam Malima alisema uongo humu Bungeni wa kusema alishuhudia kitu ambacho baadaye kwa ushahidi yeye mwenyewe aliupeleka katika Kamati niliyoiteua kunishauri na ilidhihirika kwamba yale aliyosema hayakuthibitika, yeye anadai hiyo haionyeshi uongo mimi nasema huo ni uongo. *(Makofi)*

Sasa yamedakwa na watu wengi hasa vyombo vya habari vinachonganisha kwa kila namna, tunawekewa maneno ambayo mengine hatukuyasema na kadhalika. Nakubali kabisa Bunge limepitia wakati mgumu sana kutokana na suala hili. Mimi binafsi nimesononeshwa sana na sidhani katika kipindi cha maisha yangu niliwahi kusonosheshwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Adam Kighoma Malima katika kutekeleza ule uamuzi ambao niliupitisha na kuutangaza humu, tarehe 27 Februari, 2007 nikiwa naondoka kwenda Kigali, Rwanda nilimwomba Katibu wa Bunge awasiliane naye ili nitakaporejea tarehe 04 Machi, 2007 tupange muda wa kushauriana sisi wawili Spika na Mbunge ni jinsi gani tuweze kushirikisha yule mtu wa tatu. Katibu alimpigia simu wakawasiliana na niliporudi nikataarifiwa kwamba Mheshimiwa Adam Malima kachagua yeye, sikilizeni, sikuchagua mimi kachagua yeye Jumatano tarehe 07 Machi, 2007 saa 05:00 asubuhi, taarifa nikapewa na Katibu kwamba angekuja ofisini kuniona.

Nikasubiri kwa hamu kwa sababu hatuwezi kumuingiza mtu wa tatu kabla ya sisi wenyewe hatujajua tunafanya nini na nisahihishe hapa kwamba suala hapa hakuna kuombana radhi kwamba Mheshimiwa Adam Malima amwombe radhi Ndugu Reginald Mengi au Ndugu Reginald Mengi amwombe radhi Mheshimiwa Adam Malima. Lakini ilikuwa ni suala tu kwamba haya yote yamepita sisi kama Watanzania na wenzetu hao wawili waone kwamba ni vizuri jambo hili lihitimishwe na lifikie mwisho. Saa 05:00 nilimsubiri Mheshimiwa Adam Kighoma Malima lakini hakufika, saa 05:40 Sekretari wangu Ndugu Ashura Waijaa alimpigia simu, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima akadai kwamba atafika tu mchana, mimi Spika nilikaa hadi saa 11:00 jioni lakini Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, hakufika.

Siku ya pili sikuchoka nikamwomba Katibu kwamba hata kama anayokuja kunieleza ni kuendelea kukataa si uungwana tu aje! Maana hata hiyo ni taarifa tu. Taarifa za Katibu wa Bunge kwa siku mbili zilizofuata, namba ya simu tuliyokuwa tunaitumia kumpata Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, ilikuwa haipatikani.

Basi baadaye ndiyo yamekuja haya mambo, ameandika barua kwa Chama cha Mapinduzi, kumbe hata siku ile ambayo tunatakiwa kukutana barua hiyo nimeiona ni ya tarehe 03 Machi, 2007 kwa hiyo, ilikwisha kwenda lakini sikujua hayo. Baadaye na mimi akaniandikia barua ambayo naomba nisitoe maoni lakini niseme tu kwamba imenisononesha sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa mimi nimetafakari sana suala hili, nilikuwa na njia tatu za kuweza kulishughulikia suala hili, kwanza, ni kwa mujibu wa Kanuni ya 60 ile Kanuni ndogo ya 1, naruhusiwa kumtaja Mbunge, kumtaja na nikishamtaja basi Mbunge mwingine anasimama anatoa hoja ili Mbunge huyo ajadiliwe kwa madhumuni ya kuadhibiwa. Hiyo ilikuwa inaweza kufanyika.

La pili, nilikuwa ninaweza kwa Kanuni ya 4, fasili ndogo ya 3 kufanya kama vile malalamiko ya Mheshimiwa Adam Kighoma Malima yamepotea anwani tu niyapeleke kwenye Kamati ya Kanuni ambavyo ndivyo utaratibu unahitaji. Hilo nalo likipelekwa kwenye Kamati ya Kanuni, vinaanza vikao.

Lingine ni hili alilotuletea Mheshimiwa Halima James Mdee, ndilo la tatu, kwamba ili kulihami Bunge kuhusu haki zake suala hili lijadiliwe kwa hoja inayotokana na Kanuni ya 41 (1), (2) na (3).

Waheshimiwa Wabunge, mimi ni kiongozi wenu ingawa Mheshimiwa Adam Kighoma Malima anasema kwamba tupo sawa, mimi ni Mbunge tu, Mbunge wa Urambo Mashariki, lakini nikikaa hapa ndiye Spika wa Bunge hili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawasihi kwa yafuatayo, mnielewe kwa uamuzi huu ninaotaka kuuchukua kwamba kwa sasa hivi kwenye Kamati peke yake suala hili limetumia shilingi milioni 100, taratibu hizi zote nilizozitaja nikielekeza huko itabidi tuwajibu wananchi kwamba hivi tunaendelea kutumia fedha za umma kuhusu suala hili la kusema tu kwamba Mheshimiwa Adam Kighoma Malima hakusema kweli, kasema uongo, kasema kweli.

Je, tunaweza kutumia fedha zaidi kwenye hizi Kamati kujaribu kujibu hili tu? Maana yake taabu ya danadana za Kanuni ni kwamba ni lazima liingine katika Kamati, Kamati ni watu wanakaa wanalipwa posho. Mimi niseme tu kwamba hata hizo posho za nyuma zimesababishwa na baadhi ya watu hususan Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, kupeleka mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge mashahidi ambao kwa akili yangu mimi walikuwa wala hawahusiani na suala lililokuwa mbele ya Kamati. *(Makofi)*

Watu kama Mama Mahalu, Dr. Dau na kadhalika, lakini tuliache kwa leo ila lilichukua muda mrefu mno. Sasa ukisema liende tena kwenye Kamati tunaanza mambo mapya kwa suala ambalo naliona kwa kweli halistahili kufanyika hivyo. Bunge ni chombo kikubwa na mara nyingine mkubwa ukitukanwa dawa siyo adhabu bali hata kumpuuza mtu nayo ni adhabu, kumpuuza tu! *(Makofi)*

Mimi nadhani kwa sasa hivi jamii nzima imeelewa Spika yukoje, Wabunge wakoje na Mheshimiwa Adam Kighoma Malima yukoje, jamii imekwishaelewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumechaguliwa sisi hapa tumsaidie Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwenye masuala magumu sana yanayowapata wananchi wetu. Wananchi wetu hawana maji, elimu ndiyo hiyo tunasumbuka hapa, barabara vijijini ni mbovu. Serikali imetangaza sasa hivi mkakati mpya kuhusu afya, hivi Waheshimiwa Wabunge wenzangu nikijiuliza wananchi watatuonaje kama tutaendeleza suala hili? Kwa sababu biashara kubwa inakuwa ni ya vyombo vya habari katika watu ambao wananufaika sana na hili kushinda kila mtu ni vyombo vya habari kwa sababu wanachukua tafsiri mtu hata akipiga simu ukimwambia kwamba mimi nimechoka, hiyo ni habari kesho ukurasa wa kwanza Spika amesema hataki amechoka na kadhalika.

Sasa mimi likuwa nasema kwamba hapa tulipofika nadhani tuseme inatosha, mimi suala hili nimelifunga kabisa sitaongea na Waandishi wa Habari tena, simtazamii Mbunge yeyote aliendeleze kwa sababu *agenda* yetu ni kubwa na ni ya heshima. Mwaka 2010 hatutaulizana hapa Mheshimiwa Adam Kighoma Malima alisema nini bali tutaulizana kuna visima vya maji, kuna shule, kuna barabara vijijini vimewekewa makalvati? Basi. Kwa hiyo, mtego huu mimi nauona ni mtego kwa sababu hata huku sura inayochukua ambayo ni nje kabisa si sahihi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mtego huu hata kidogo Wabunge mnajua nani anatetea haki za Demokrasi ya Bunge hapa, Bunge hili bado ndiyo mwaka wa pili. Unajua wananchi wakishatudharau mwaka wa pili kufika mwaka wa tatu au wa nne tutakuwa *irrelevant* na hakuna kitu kibaya kama kiongozi kuonekana *you are irrelevant,* hamna faida, watu wana msongamano Dar es Salaam, misururu ya magari na kadhalika basi tutafute dawa ya matatizo ya wananchi tuache kabisa hili suala la Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, mimi nimelifunga kabisa na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane tu na mwenzetu, mara nyingine mtu anahitaji tu msaada siyo adhabu, kwa hiyo, tusaidiane na mwenzetu ili twende naye vizuri, ni kijana mzuri tu nadhani akisaidiwa kwa ushauri nasaha itaweza kusaidia tukaenda vizuri. *(Makofi)*

Baada ya maneno hayo napenda kusema mimi mjadala wa Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, nimeufunga na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge mnisaidie katika hili ili turejeshe hadhi ya Bunge siyo kwa kumwadhibu ila kwa kumsaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kutamka sasa kwamba naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho asubuhi saa 03:00 asubuhi.

*(Saa 05.12 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 11 Aprili, 2007 Saa 03.00 asubuhi)*